

Kadi ya kupunza malipo (Concession Card)



Concession Cards - Swahili

Pensioner Concession Card

Pensioner Concession Card ni kadi ambayo inatolewa kwa wale walio kwenye penshoni na wale wanaopata malipo ya Parenting Payment Single, Mature Age Allowance, Mature Age Partner Allowance na Carer Payment. Kadi hii pia inatolewa kwa watu waliozidi umri sitini na wamekuwa wakipokea malipo mengine kwa zaidi ya miezi tisa. Watu walio angaliwa kuwa kwa kiwango fulani wanaweza kufanya kazi na wanapokea malipo ya Newstart Allowance, Youth Allowance (mengine), na Parenting Payment (mshirika) pia wanaweza kupata Pensioner Concession Card.

Pensioner Concession Card inawapa wale walio na kadi hii concessions za ziada kitaifa na katika serekali kienyeji. kuna tofauti katika serekali mbali mbali kwa kupunguza malipo yako ya nyumba, kupunguza malipo yako ya maji, kupunguza malipo yako ya umeme au gesi, kupunguza nauli ya tiketi yako ya kusafiri kupitia umma, kupunguza malipo yako ya uandikishaji wa gari, na tiketi moja au zaidi ya kusafiri bure kupitia reli kila mwaka. Sehemu zingine za serekali wana concessions tofauti za afya, matumizi ya nyumbani, masomo na burudani.

Health Care Card

Health Care Card inatolewa kwa wale ambao wanapokea malipo zingine za Centrelink pamoja na Newstart Allowance, Special Benefit, Sickness Allowance, Partner Allowance na kikundi fulani ya watu wanaopokea Youth Allowance. Kadi hii pia inatolewa kwa wale walio na mshara duni kwa muda wa miezi sita, na chini ya masharti kadha, kwa wasaidizi wanaochunga ama kuwaangalia watu ambao sio familia yao. Watu walio na miaka kumi na sita hadi ishirini na tano ambao ni wanafunzi wa kila siku yaani full time, wana ulemavu au wako katika hali ambayo wanahitaji kuwa na mtu wa kuwatunza, ambaye aliweza kupata malipo ya kuwatunza ijulikanayo kama carer allowance (mtoto) siku ile kabla ya mtoto kufika miaka kumi na sita, pia wanaweza kupata kadi ya health care. Katika hali hii, mshara wako haita kaguliwa kwa njia ijulikanayo kama income test.

Concession ya kupunguza bei ya dawa katika maduka ya dawa iko pamoja na Health Care Card. Pia kuna kiasi fulani ya concession inayotolewa kwa mahitaji ya nyumbani, masomo, burudani na usafiri.

Commonwealth Seniors Health Card

Commonwealth Seniors Health Card inatolewa kwa watu ambao wako katika umri wa penshoni ya wazee lakini hawafaulu kupata penshoni. Unaweza kutuma ombi ya kupata kadi hii peke yake bila kuomba penshoni. Kutuma ombi hii, ni lazima uwe mkazi wa Australia na unaishi Australia. Utahitajika kuwa na Tax file namba yako pamoja na Tax file namba ya mshirika wako au uwaeleze ni kwa nini hauwezi kuwapa maagizo hayo. Utahitajika kufanya testi ya mshara yako ijulikanayo kama income test, ili kuangalia mshara wako. Hata hivyo hauta hitajika kuwapa maelezo kuhusu vifaa/mitaji yako.

Ikiwa unasafiri kwende nga'mbo au nje ya Australia kwa muda isiyozidi wiki kumi na mbili, hautapoteza kadi yako ya Commonwealth Seniors Health Card, lakini ni lazima uwaeleze Centrelink kabla ya kusafiri.

Centrelink inaweza kutoa fomu ya Confirmation of Concession Card Entitlement kwa wateja ambao hawawezi kungoja kadi yao mpya ya concession inayotolewa kwao kwa kawaida.

Jinsi ya kujua mengi zaidi

Kuongea na Centrelink katika Kiswahili, piga simu **13 1202***. Maelezo katika Kiswahili yanaweza kupatikana kwa mtandao **www.centrelink.gov.au**

* Malipo ya kupiga simu kutoka simu yako ya nyumbani kwa simu za Centrelink namba "13" huwa tofauti kutegemea na mtoaji wa huduma ya simu yako. Simu kwa namba "1800" kutoka simu yako ya nyumbani ni bure hazilipishwi. Simu kutoka kwa simu ya watu wote na simu ya mkono hulipishwa bei ya juu.

